

“Biblia yasemaje?...”
Yesu aliyachukualiaje maandiko?
Sehemu ya nane

“Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mlima mrefu mno, akamwonyesha milki zote za ulimwengu, na fahari yake, akamwambia, haya yote nitakupa, ukianguka kunisijudia. Ndipo Yesu akamwambia, Nenda zako, Shetani; maana imandikwa Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake” Matthew 4:9-10.

Shetani kwa mara ya pili alishindwa kumshawishi Yesu atende dhambi dhidi ya Babaye. Sasa katika Mathayo 4:8-10, Shetani anamjaribu Yesu kwa mara ya tatu, na tena Yesu anajibu kwa kutumia maandiko kwa kutupa sisi tafsiri ya kimaandiko tunayotakiwa kuiga na kufuata.

Kisha shetani akamchukua Yesu mpaka kwenye mlima mrefu na akamshawishi kwa kumuahidi heshima ya kidunia na tunu, kwa msingi wa gharama ya Kristo kuinama kumsujudu Shetani. Kama alivyofanya awali, Yesu alinukuu andiko kutoka katika Kumbukumbu la Torati 6:13 na kumwambia shetani kuwa tunatakiwa kumsujudia na kumtumikia Mungu peke yake.

Yesu alielewa sheria za kujua maana katika kutafsiri maandiko. Mungu anaposema tufanye jambo fulani kwa namna fulani, humaanisha kuwa hakuna namna nyingine itakayofaa. Mungu alipowaumba Adamu na Hawa ili wamtumikie, kwa wao kumtumikia mwingine awaye yote ilikuwa ni dhambi. Mungu anapotuambia tumtumikie, hahitaji kutaja wengineo tusiotakiwa kutumikiwa. Hapa Yesu alitoa amri akimaanisha nani wa kumtumikia, amri ambayo huweka kando kinginecho!

Kama watu wenyewe uwezo wa akili wa kawaida. Tunaelewa sheria za kujua maana. Mgahawani unapokuta choo kimeandikwa “wanawake” tunaelewa kuwa maelezo huwakataza nani? Wakati huo huo mgahawani tukiagiza kikombe cha kahawa, hapo tunakuwa tumekataa nini? Tunakuwa tumekataa kinginecho kiwacho chote, chai, mnofu, mayai, mpira, alizeti. Tunazielewa hizi sheria katika maisha yetu ya kila siku. Hivi, ndivyo tunavyoelewa linapofika neno la Mungu? Enyi watu wema, Mungu akisema kitu, hahitaji tena kuanza kutaja asichokihusisha, na kwa kweli kila kitu ambacho hajataja anakuwa amekikataa

Kazi yetu ni kutii tu alichosema na kukaa mbali na ambapo hakuna “asema Bwana.”

Je unafuata kielelezo cha Yesu katika maisha yako ya kila siku na Ibada?